



Org. Nr:802516-6979

Kumb.TDC20230330/01

TANGAZO KWA WANACHAMA TDC GLOBAL NA
DIASPORA WATANZANIA

Baraza la diaspora wa Tanzania duniani - TDC Global, linapenda kuwakumbusha wanachama na diaspora wa Tanzania kuwa, litafanya mkutano mkuu na uchaguzi wa viongozi wake taraha 11 na 12 Julai 2023 nchini Tanzania. Diaspora wote mnakaribishwa kushiriki katika mkutano, utaratibu wa kujisajili kwa ushiriki utatangazwa baadaye.

Kushiriki katika uchaguzi wa viongozi unatakiwa kuwa ni mwanachama hai – financial member (kwa mujibu wa katiba #10.1 a na c). Kutokana na umuhimu wa uchaguzi, uongozi wa TDC Global umeboresha ulipaji ada kuwa rahisi na rafiki kwa wanachama, lipia ada yako ili waweza kufaidika na haki na faida za mwanachama (kwa mujibu wa katiba # 10.4 a,b,c,d, & e),

Wanachama na diaspora mnaojiunga mnaweza kulipia ada zenu kutokea nchi yeyote duniani, kupitia kiunganisha hiki: https://bit.ly/TDCGlobal_Membership_Fees. Weka taarifa zako, chagua kiwango cha ada unayopendezwa kulipia, miezi mitatu USD 15, miezi sita USD 30 au mwaka USD 60, kisha kamilisha malipo. TDC Global inawaomba mtakaofikiwa na taarifa hii, kuwapatia diaspora wengine katika nchi zenu za makazi.

Kwa wanachama wasio na kumbukumbu au uhalisia wa malipo yao ya ada, wanaombwa kuwasiliana na katibu hazina Bi. Seynab Haji kupitia barua pepe hazina@tdcglobal.org na simu +46763920337. Taarifa zaidi za mkutano mkuu zitaendelea kutolea kadri zinavyokamilika au kwa maombi yatakayowasilishwa TDC Global kupitia barua pepe: info@tdcglobal.org

Uongozi wa TDC Global unatakuliza shukrani kwa ushirikiano mnaotupatia. *Tukutane Tanzania tarehe 11 na 12 Julai 2023*. Mungu ibariki afrika, Munga ibariki Tanzania.

Diaspora na Nyumbani

Seynab Haji
Katibu Hazina
TDC Global
2023-03-30

